**HOTUBA YA IJUMAA**

**التكاتف الوطني في التعامل مع الأزمات**

**Mshikamano wa kitaifa katika kupambana na matatizo**

**Imefasiriwa**

**na**

**profesa Ayman Alasar**

Shukrani zote anastahiki Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe vyote Mwenye kusema ndani ya Kitabu chake Kitukufu: **وَتَعاوَنُوا عَلَى البِرِّ وَالتَّقْوَى** {**Na shirikianeni kwenye mambo mema na ucha-Mungu**}. Ninashuhudia kuwa hakuna mola wa haki isipokuwa ni Mwenyezi Mungu peke yake hana mshirika, na ninashuhudia kuwa Mtume wetu Muhammad SAW ni mja wake na Mtume wake. Ewe Mwenyezi Mungu peleka rehma amani na baraka kwake na kwa watu wake na Maswahaba zake na wale waliowafuata kwa wema mpaka siku ya kiyama.

**Baada ya utangulizi huo**:

Jamii iliyobora ni jamii yenye mshikamano na ushirikiano na hasa kipindi cha nyakati za matatizo, na Mtume wetu SAW amezielezea jamii bora kwa kauli yake:

**مَثَلُ المُؤْمِنِينَ فِي تَوَادِّهِمْ وَتَرَاحُمِهِمْ وَتَعاطُفِهِمْ كَمَثَلِ الجَسَدِ، إِذَا اشْتَكَى مِنْهُ عُضْوٌ تَداعَى لَهُ سَائِرُ الجَسَـدِ بِالسَّهَرِ وَالحُمَّى.**

*"Mfano wa Waumini katika kupendana kwao na kuoneana kwao huruma ni kama mfano wa mwili, pindi kiungo kimoja kinapopata maumivu basi mwili wote hupata homa*" na anasema tena: **الْمُؤْمِنُ لِلْمُؤْمِنِ كَالْبُنْيَانِ يَشُدُّ بَعْضُهُ بَعْضًا، وَشَبَّكَ بَيْنَ أَصَابِعِه** "*Muumini kwa Muumini ni kama majengo mawili yaliyoshikana yenyewe kwa yenyewe, na akashikanisha vidole vyake*".

Na fiqhi ya matatizo inahitaji mshikamano wa kijamii kupitia mambo mengi miongoni mwa hayo ni: Kujiweka mbali na aina zote za fitina ukiritimba na matumizi mabaya, kwani dini imekataza kabisa vitu hivyo na imekuja na makatazo makali kuhusu kughushi kwa sura zake zote, na katika Aya ya kwanza kuteremka Madina ni kauli ya Mola Mtukufu:

وَيْلٌ لِلْمُطَفِّفِينَ * الَّذِينَ إِذَا اكْتَالُوا عَلَى النَّاسِ يَسْتَوْفُونَ * وَإِذَا كَالُوهُمْ أَوْ وَزَنُوهُمْ يُخْسِرُونَ * أَلَا يَظُنُّ أُولَئِكَ أَنَّهُمْ مَبْعُوثُونَ * لِيَوْمٍ عَظِيمٍ * يَوْمَ يَقُومُ النَّاسُ لِرَبِّ الْعَالَمِينَ.

{**Ole wao hao wapunjao! * Ambao wanapo jipimia kwa watu hudai watimiziwe * Na wao wanapo wapimia watu kwa kipimo au mizani hupunguza * Kwani hawadhani hao kwamba watafufuliwa * Katika Siku iliyo kuu * Siku watapo msimamia watu Mola Mlezi wa walimwengu wote**}. Na Mola Mtukufu anasema kupitia ulimi wa Nabii Shuaibi *amani ya Mungu iwe kwake*:

وَيَا قَوْمِ أَوْفُوا الْمِكْيَالَ وَالْمِيزَانَ بِالْقِسْطِ وَلاَ تَبْخَسُوا النَّاسَ أَشْيَاءَهُمْ وَلاَ تَعْثَوْا فِي الأَرْضِ مُفْسِدِينَ.

{**Enyi watu kimilisheni kipimo na mizani kwa usawa na wala musiwapunje watu vitu vyao na wala musifanya uharibifu duniani**}. Na anasema Mtume SAW:

مَنْ غَشَّنَا فَلَيْسَ مِنَّا.

"*Mwenye kutufanyia udanganyifu basi huyo si katika sisi*".

Kama vile Sharia imekataza aina zote za ukiritimba na matumizi mabaya ikiwa ndani yake ni pamoja na kuchezea vyakula vya watu na nguzo za maisha yao pamoja na kuzishikilia ili kufikia mafanikio haramu kwa kutumia matatizo ya watu na shida zao ambapo Mola Mtukufu Anasema:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لاَ تَأْكُلُوا أَمْوَالَكُمْ بَيْنَكُمْ بِالْبَاطِلِ إِلاَّ أَنْ تَكُونَ تِجَارَةً عَنْ تَرَاضٍ مِنْكُمْ وَلاَ تَقْتُلُوا أَنْفُسَكُمْ إِنَّ اللَّهَ كَانَ بِكُمْ رَحِيمًا.

{*Enyi mlioamini musile mali zetu kati yenu kwa ubatilifu isipokuwa iwe ni biashara ya maridhiano kati yenu wala musijiue wenyewe hakika Mwenyezi Mungu amekuwa ni mpole*}. Na anasema Mtume SAW:

**كُلُّ الْمُسْلِمِ عَلَى الْمُسْلِمِ حَرَامٌ، دَمُهُ، وَمَالُهُ، وَعِرْضُهُ.**

"*Kila Muislamu kwa Muislamu haramu damu yake mali zake na heshima yake*". Na anasema tena Mtume: **لَا يَحْتَكِرُ إِلَّا خَاطِئٌ** "*Hafanyi ukiritimba isipokuwa ni anafanya makosa*" mkiritimba hana uzalenda wala utaifa kwa sababu ubinfsi wake ameufanya kuwa zaidi ya mazingatio ya dini au taifa au ubinadamu, hivyo anastahiki hasira za Mwenyezi Mungu Mtukufu na hasira za watu.

Lau mkiritimba atafahamu kuwa mali ambayo anaipata kwa ukiritimba wake itakuwa ni janga kwake siku ya kiyama na kuwa hii ni adhabu kwa hiyo dhuluma, ambapo Mola Mtukufu anasema: **وَمَنْ يَغْلُلْ يَأْتِ بِمَا غَلَّ يَوْمَ الْقِيَامَةِ** {**Na mwenye kufanya ukiritimba basi siku ya kiyama ataletwa na kile alichokifanyia ukiritimba**}. Na Mtume SAW anasema: **الْجَالِبُ مَرْزُوقٌ وَالْمُحْتَكِرُ مَلْعُونٌ** "*Asiyefanya ukiritimba ni mwenye kuruzukiwa na mkiritimba ni mwenye kulaaniwa*".

Ama mtu tajiri mwenye uzalendo na mkweli ni yule asiyefanya udanganyifu haghushi wala kufanya usaliti bali utaifa na uzalendo wake unamsukuma hasa wakati wa matatizo kupunguza sehemu ya faida zake kusaidia kuwapunguzia watu matatizo, hakuna shaka kuwa hilo ni katika huruma ambao unapelekea thawabu kwake, na Mwenyezi Mungu Mtukufu ameahidi kupitia ulimi wa Mtume wake SAW kuwa tajiri mkweli ana malipo mkubwa ambapo Mtume SAW anasema:

**التَّاجِرُ الصَّدُوقُ الأَمِينُ مَعَ النَّبِيِّينَ، وَالصِّدِّيقِينَ، وَالشُّهَدَاءِ.**

"*Tajiri mkweli muaminifu yupo pamoja na Mitume wakweli na mashahidi*".

Na Mtume SAW anasema: **رَحِمَ اللهُ رَجُلاً سَمْحًا إذا باعَ، وإذا اشْتَرى، وإذا اقْتَضى** "*Mwenyezi Mungu humfanyia huruma mtu husamehe wakati wa kuuza na pindi anaponunua na pindi anapotumia*".

## HOTUBA YA PILI.

Shukrani zote anastahiki Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe vyote, rehma na amani zimwendee Mtume wa mwisho Mtume Muhammad SAW pamoja na watu wake na Maswahaba zake wote.

Kwa hakika nyakati za matatizo zinahitaji kujitoa kwa ajili ya watu na wala si kuzitumia vibaya kama fursa, kama vile zinahitaji huruma na wala si roho mbaya na ubinafsi, ambapo Mtume SAW anasema:

**مَا آمَنَ بِي مَنْ بَاتَ شَبْعَانَ وَجَارُهُ جَائِعٌ إِلَى جَنْبِهِ وَهُوَ يَعْلَمُ بِهِ.**

"*Hajaniamini mimi yule ambaye analala akiwa ameshiba jirani yake wa karibu ana njaa hali ya kuwa anajua hailo*". Kama vile nyakati hizo za shida na matatizo zinahitaji pia huruma kufanya juhudi na kutoa, ambapo Mwenyezi Mungu Mtukufu Anasema: **وَيُؤْثِرُونَ عَلَى أَنفُسِهِمْ وَلَوْ كَانَ بِهِمْ خَصَاصَةٌ وَمَن يُوقَ شُحَّ نَفْسِهِ فَأُولَئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ** { **Na wanawapendelea wenzao zaidi kuliko nafsi zao pamoja na wao kuwa ni wenye kuhitaji, na wenye kuondoshewa ubahili kwenye nafsi zao basi hao ndio waliofaulu**} na Mtume SAW anasema:

**إِنَّ الأَشْعَرِيِّينَ إِذَا أَرْمَلُوا فِي الغَزْوِ، أَوْ قَلَّ طَعَامُ عِيَالِهِمْ بِالمَدِينَةِ جَمَعُوا مَا كَانَ عِنْدَهُمْ فِي ثَوْبٍ وَاحِدٍ ثُمَّ اقْتَسَمُوهُ بَيْنَهُمْ فِي إِنَاءٍ وَاحِدٍ بِالسَّوِيَّةِ، فَهُمْ مِنِّي وَأَنَا مِنْهُمْ.**

"*Watu wa kabila la Ash-ary pindi wanapoishiwa au kupungukiwa chakula wakati wa vita kwa familia zao huko Madina hukusanya walichonacho kwenye nguo moja kisha wanagawa kati yao kwenye chombo kimoja kwa usawa, basi wao ni katika mimi na mimi ni katika wao*".

Hakuna shaka kuwa mshikamano huu una nafasi kubwa katika kuimarisha mfungamano wa kijamii na kibinadamu, na kukuza undugu na upendo kwa watu ndani ya jamii, kwa sababu hiyo Sharia ya Kiislamu imekuja kuhimiza hilo ambapo Mwenyezi Mungu Mtukufu Anasema: **وَتَعَاوَنُوا عَلَى الْبِرِّ وَالتَّقْوَى وَلَا تَعَاوَنُوا عَلَى الْإِثْمِ وَالعُدْوَانِ** {**Na shirikianeni kwa mambo mema na ya ucha-Mungu, na wala musishirikiane kwenye dhambi na uadui**}, na mshikamano huu unakuwa wazi zaidi kupitia pia kutoa kwenye mambo mbalimbali yak heir na hasa kama yanayohusiana na utoaji chakula na kusaidia mahitaji ya watu masikini, ambapo Mwenyezi Mungu Mtukufu Anasema katika wasifu wa watu wema:

**وَيُطْعِمُونَ الطَّعَامَ عَلَى حُبِّهِ مِسْكِينًا وَيَتِيمًا وَأَسِيرًا* إِنَّمَا نُطْعِمُكُمْ لِوَجْهِ اللَّهِ لاَ نُرِيدُ مِنكُمْ جَزَاءً وَلاَ شُكُورًا * إِنَّا نَخَافُ مِن رَّبِّنَا يَوْمًا عَبُوسًا قَمْطَرِيرًا * فَوَقَاهُمُ اللَّهُ شَرَّ ذَلِكَ الْيَومِ وَلَقَّاهُمْ نَضْرَةً وَسُرُورًا* وَجَزَاهُمْ بِمَا صَبَرُواْ جَنَّةً وَحَرِيرًا.**

{**Na huwalisha chakula, juu ya kukipenda kwake, masikini, na yatima, na wafungwa * Hakika sisi tunakulisheni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Hatutaki kwenu malipo wala shukrani * Hakika sisi tunaiogopa kwa Mola wetu Mlezi hiyo siku yenye shida na taabu * Basi Mwenyezi Mungu atawalinda na shari ya siku hiyo, na atawakutanisha na raha na furaha * Na atawalipa Bustani za Peponi na nguo za Hariri kwa vile walivyo subiri**}. Na Mola Mtukufu anasema tena:

**أَوْ إِطْعَامٌ فِي يَوْمٍ ذِي مَسْغَبَة* يَتِيمًا ذَا مَقْرَبَةٍ* أَوْ مِسْكِينًا ذَا مَتْرَبَةٍ.**

{**Au kumlisha chakula siku ya njaa * Yatima ambaye ni ndugu * au masikini aliyevumbini**}. Na Mtume SAW anasema:

**أَطْعِمُوا الطَّعَامَ، وَصِلُوا الْأَرْحَامَ، وَصَلُّوا بِاللَّيْلِ وَالنَّاسُ نِيَامٌ تَدْخُلُوا الْجَنَّةَ بِسَلَامٍ.**

"*Lisheni chakula na unganisheni undugu na swalini usiku watu wakiwa wamelala mutaingia Peponi kwa amani*". Na anasema tena: **خِيَارُكُمْ مَنْ أَطْعَمَ الطَّعَامَ** "*Mbora wenu ni yule mwenye kulisha chakula*".

**Ewe Mwenyezi Mungu ilinde nchi yetu pamoja na nchi zengine za Kiislamu na Kiarabu.**